


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

WAOMBAJI WALIODAHILIWA ZAIDI YA CHUO KIMOJA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inatangaza kuwa udahili kwa awamu ya kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2019/2020 umekamilika. Majina ya waombaji waliochaguliwa katika awamu ya kwanza yameshatangazwa na vyuo husika.

Hata hivyo baadhi ya waombaji wamedahiliwa chuo zaidi ya kimoja. Hivyo wanasisitiza **kuthibitisha** udahili wao katika chuo kimoja kuanzia tarehe **20 hadi 29 Agosti 2019**, kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba ya simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyochaguliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha.

Uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti waombaji walizoitumia wakati wa kuomba udahili kupitia vyuo husika. Orodha

ya majina ya waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

Kutokana na baadhi ya waombaji kutochaguliwa katika awamu ya kwanza ya udahili kwa sababu mbali mbali, Tume inatangaza dirisha la maombi ya udahili awamu ya pili kuanzia tarehe **21 hadi 29 Agosti, 2019** ili kuruhusu makundi yafuatayo kuomba udahili:

- Waombaji waliokosa nafasi kwenye awamu ya kwanza;
- Waombaji wa kidato cha sita na stahahada walioshindwa kuomba katika awamu ya kwanza;
- Waombaji waliomaliza mitihani ya “Cambridge” mwaka 2019 na matokeo yao yameshatoka; na
- Waombaji waliokuwa wamedahiliwa miaka ya nyuma na kuacha au kukatisha masomo.

Aidha, Tume inapenda kuisisitiza kuwa utaratibu wa kutuma maombi ni ule ule wa kutuma maombi moja kwa moja vyuoni kama ilivyokuwa katika awamu ya kwanza ya udahili. ***Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili (ama kujithibitisha) yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyo husika na siyo TCU.***

Imetolewa na:



Dr. Kokuberwa Katunzi Mollel

KNY: Katibu Mtendaji

Tume ya Vyo Vikuu Tanzania

20 Agosti, 2019